# مَا لَا يُؤَثِّرُ فِي

# الصِّيَامِ

# MAMBO YASIYOHARIBU

# SAUMU/FUNGA

Mwandishi:

Dr. Muhammad Bin Ghayth Ghayth

Tarjama:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

بسم الله الرحمن الرحيم

Hakika miongoni mwa hukumu za Kisheria ambazo inapasa kwa mfungaji kujifunza, ni kujua mambo ambayo ni halali kuyafanya na wala hayaathiri chochote katika saumu yake, ili asije akaitumbukiza nafsi yake katika tabu na kuifanyia uzito, na ili afahamu kwamba Dini ya Allaah ni nyepesi, kwa hiyo miongoni mwa mambo yasiyoharibu Saumu/Funga ni haya yafuatayo:

### 1. KUPIGA MSWAKI:

Imepokewa kutoka kwa Aisha-Allaah amridhie- amesema: Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«السِّوَاكُ مَطْهَرَةٌ لِلْفَمِ، مَرْضَاةٌ لِلرَّبِّ»

**[Mswaki ni wenye kutwaharisha sana kinywa, ni wenye kumridhisha sana Mola][1].**

Na imepokewa kutoka kwa Abu Huraira -Allaah amridhie- amesema: Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«لَوْلا أَنْ أَشُقَّ عَلَى أُمَّتِي، لَأَمَرْتُهُمْ بِالسِّوَاكِ عِنْدَ كُلِّ صَلَاةٍ»

**[Lau nisingechelea kuutia umma wangu katika tabu (mashaka au uzito), ningeliwajibisha kwao kupiga mswaki wakati wa kila swala][2].** Swala zote za faradhi na sunna

Na imepokewa kutoka kwa Aamir Bin Rabia-Allaah amridhie- amesema:

«رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَا لَا أَعُدُّ، وَمَا لَا أُحْصِي «يَسْتَاكُ وَهُوَ صَائِمٌ»

Nilimuona Mtume -Swala na Salamu zimshukie- **[Anapiga mswaki hali ya kuwa amefunga],** ni mara nyingi, siwezi kuhesabu idadi wala kudhibiti: [3].

---

1- Musnad Ahmad (Jz. 1, Uk. 116), na Imam Bukhari ameitaja kwa Ta'liiq kwa tamko la Jazmi katika sahihi yake.
2- Musnad Ahmad (Jz. 2, Uk. 43), hadithi namba (607).
3- Musnad Ahmad (Jz. 24, Uk. 447), hadithi namba (15678).

Na pia inafaa kutumia dawa ya meno, lakini inampasa mtu achukue tahadhari, ili isije ikapitiliza na kuingia tumboni mwake.

## 2. KUSUKUTUWA NA KUPANDISHA MAJI PUANI KWA SHARTI LA KUTOFANYA MUBAALAGHA/KUBALIGHISHA[4]:

Imepokewa kutoka kwa Laqit Bin Swabura -Allaah amridhie- amesema: Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«وَبَالِغْ فِي الِاسْتِنْشَاقِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ صَائِمًا»

**[Na fanya mubalaagha katika kupandisha/kuvuta maji puani, isipokuwa ukiwa umefunga][5].**

Katika hadithi hii kuna katazo la mtu kuyavuta maji wakati wa kusukutuwa au kupandisha maji puani kwa mtu aliyefunga, ili isije yakapitiliza mpaka tumboni, pia kusukutuwa asiyafikishe mbali, lakini endapo yalipita sehemu ya maji hayo mpaka tumboni kwa sababu ya kushindwa kuyazuia, bado (saumu yake) haijabatilika, kwa kauli ya wengi katika Maulamaa.

## 3. KUOGA AU KUJIMWAGIA MAJI KICHWANI (KWA SABABU YA KIU/JOTO KALI):

Amepokea Abubakar Bin Abdil Rahman, kutoka kwa baadhi ya Maswahaba wa Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

**لَقَدْ رَأَيْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِالْعَرْجِ، «يَصُبُّ عَلَى رَأْسِهِ الْمَاءَ مِنَ الْعَطَشِ» - أَوْ مِنَ الْحَرِّ**

Hakika nilimuona Mtume -Swala na Salamu zimshukie- katika sehemu inayoitwa 'Arju[6]: **[Anakimwagia maji kichwa chake kutokana na kiu, au joto (kali)][7].[8]**

---

[4]- Kufanya mubalagha wakati wa kusukutuwa au kuvuta maji puani, ni kuyapeleka maji mbli

[5]- Sunan Abi Daud (142).

[6]- 'Arju ni Kijiji kwa masiku kadhaa kutoka Madina.

[7]- Musnad Ahmad (Jz. 25, Uk. 241), hadithi namba (15903), Abu Daud (2365).

[8]- Amesema Ibn Qudama: [Al Mughni: Jz: 3, Uk. 124] **"Wala Hapana vibaya kwa mfungaji kuoga".** "وَلَا بَأْسَ أَنْ يَغْتَسِلَ الصَّائِمُ"

## 4. KUCHELEWESHA KUOGA JANABA MPAKA ASUBUHI:

Imepokewa kutoka kwa Aisha na Ummu Salama -Allaah awaridhie-: kwamba alikuwa Mtume-Swala na Salamu zimshukie-

«يُدْرِكُهُ الفَجْرُ وَهُوَ جُنُبٌ مِنْ أَهْلِهِ، ثُمَّ يَغْتَسِلُ، وَيَصُومُ»

**[Unamdiriki yeye wakati wa alfajri akiwa ana janaba kwa (kukutana) na mmoja kati ya wakeze, kisha anaoga na anafunga][9].**

Amesema Ibn Hajar-Allaah amrehemu-: **[Jumhuri ya Maulamaa (Maulamaa wengi) wanaona linafaa hilo kwa hali yoyote][10].** Anakusudia kufaa kufunga kwa mtu aliyeamka akiwa na janaba (sawa ameota au alifanya jimai).

Kadhalika mwanamke mwenye Hedhi au Nifasi, ikiwa damu imekata usiku kabla ya kuchomoza alfajri, itafaa kwao kuchelewesha kuoga mpaka asubuhi na itajuzu kwao kufunga katika siku hiyo.

## 5. KUFANYA HIJAMA/KUUMIKA/KUPIGA CHUKU/KUGONGA MSHIPA:

Imepokewa kutokwa Ibn Abbas -Allaah amridhie- amesema:

«أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ احْتَجَمَ وَهُوَ مُحْرِمٌ، وَاحْتَجَمَ وَهُوَ صَائِمٌ»

**[Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alifanya Hijama hali ya kuwa amefunga][11].**

Amesema Ibn Hajar -Allaah amrehemu-: **[Ama Hijama, (kauli wa Maulamaa) wengi ni kwamba haifunguzi kwa hali yoyote][12].** Sawa ni damu chache au nyingi.

---

[9]- Bukhari (1926) na Muslim (76).
[10]- Fa-hul Baari (Jz. 4, Uk. 142).
[11]- Bukhari (5694).
[12]- Fat-hul Baari (Jz. 4, Uk. 174).

Lakini ni karaha endapo atahofia yule mwenye kufunga kwamba atadhoofika sana ikiwa atatoa damu.

Kutoka kwa Thabit Al Bunani -Allaah amrehemu- Aliulizwa Anas Ibn Malik -Allaah amridhie-: **[Je, mlikuwa mnaona karaha kwa mtu aliyefunga kufanya Hijama? Akasema: Hapana, isipokuwa (tukiona karaha) kwa ajili ya kuhofia kudhoofika]**[13].

Na kwa kufanyia kiasi cha Hijama, itafaa pia kutoa damu kwa ajili ya vipimo (kama Malaria n.k), au kujitolea kwa kumsaidia mtu mwingine, lakini iliyo bora ni mtu kusubiri mpaka jioni baada ya kufungua/kufutari.

## 6. KUONJA LADHA YA CHAKULA ENDAPO ITAHITAJIA:

Amesema Ibn Abbas-Allaah amridhie-:

"لاَ بَأْسَ أَنْ يَتَطَعَّمَ القِدْرَ "

**[Hapana vibaya kuchukua chakula kwenye chungu na kutia kinywani kwa ajili ya kuonja]**[14].

Na amesema Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-: **[Ni karaha (kwa mfungaji) kuonja chakula bila ya kuhitajia hilo, lakini hakufunguzi, na akiwa amehitajia (hukumu yake) ni sawa na kusukutuwa maji (hakufunguzi)]**[15].

Ataonja kwa kutumia ncha yake ya ulimi tu, pasi na kumeza.

## 7. KUBUSU NA KUKUMBATIA KWA MFUNGAJI:

Amesimulia Aisha-Allaah amrdihie- kwamba alikuwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie:

---

[13]- Bukhari (1940).
[14]- Bukhari (Jz. 3, Uk. 30) chini ya mlango: **[mlango wa (kufaa) kuoga kwa mfungaji].**
[15]- Majmuu' al Fataawa (Jz. 25, Uk. 266).

«يُقَبِّلُ وَيُبَاشِرُ وَهُوَ صَائِمٌ، وَكَانَ أَمْلَكَكُمْ لِإِرْبِهِ»

**"Anabusu na kukumbatia (wakeze) hali ya kuwa amefunga, (lakini) alikuwa anamiliki zaidi matamanio yake[16]"[17].**

Na katika riwaya nyingine:

«كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُقَبِّلُ، فِي رَمَضَانَ، وَهُوَ صَائِمٌ»

**"Alikuwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- anabusu (wakeze) katika (mchana) wa Ramadhani na hali ya kuwa amefunga"[18].**

## 8. KUJIPAKA MAFUTA, KUJITIA MANUKATO, KUPAKA WANJA N.K:

Amesema Ibn Masoud -Allaah amrehemu-: **[Atakapoamka mmoja wenu akiwa amefunga, (Hapana vibaya) kujipake mafuta na kuchana nywele zake][19].**

Amesema Imam Bukhari-Allaah amrehemu-:

"وَلَمْ يَرَ أَنَسٌ، وَالحَسَنُ، وَإِبْرَاهِيمُ بِالكُحْلِ لِلصَّائِمِ بَأْسًا"

**"Na Anas, Al Hassan na Ibrahim hawakuona ubaya wowote kwa mfungaji kupaka wanja"[20].**

## 9. KUTUMIA DAWA YA MATONE (SYRUP) MACHONI, MASIKIONI NA PUANI:

Kauli yenye nguvu ni kwamba kutia dawa ya matone katika macho haifunguzi kwa hali yoyote, kwa sababu macho si njia ya kupita kitu kwenda tumboni, kadhalika kujitia matone masikioni.

---

16- Amesema Imam Nawawi -Allaah amrehemu-:

ذَكَرْنَا أَنَّ مَذْهَبَنَا كَرَاهَتُهَا لِمَنْ حَرَّكَتْ شَهْوَتَهُ وَلَا تُكْرَهُ لِغَيْرِهِ وَالْأَوْلَى تَرْكُهَا

**[Tumetaja kwamba madhehebu yetu jambo hilo ni karaha kwa yule ambaye (jambo hilo) litachochea matamanio yake, na wala si karaha kwa asiyekuwa huyo, na iliyo bora zaidi ni kuliacha jambo hilo].** Al Majmuu' (Jz. 6, Uk. 355).

17- Bukhari (1927) na Muslim (1106).

18- Muslim (71).

19- Bukhari (Jz. 3, Uk. 30).

20- Bukhari (Jz. 3, Uk. 30).

Ama kujitia dawa ya matone puani, jambo hilo halifai kwani linapelekea kubatilika kwa saumu ya mfungaji, kwa sababu pua ni njia ya kupita kitu kuelekea tumboni, ndio maana Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«وَبَالِغْ فِي الِاسْتِنْشَاقِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ صَائِمًا»

**[Na fanya mubalaagha katika kupandisha/kuvuta maji puani, isipokuwa ukiwa umefunga][21].** Anakusudia wakati wa kutawadha.

## 10. KUCHOMA SINDANO:

Haitabatilika saumu ya mfungaji kwa kuchoma sindano aina yoyote kwa ajili ya tiba, na hii ndio kauli yenye nguvu, isipokuwa sindano ya kulisha, kama vile sindano ya (vitamin c) inafunguza, kwa sababu inachukua nafasi saw ana mtu aliyekula chakula.

Wabillaahi Ttaufiq.

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**
**19/sha'ban/1445H-29/02/2024M**
**Tanga pongwe**
**Tanga.**

[21]- Sunan Abi Daud (142).